# *Melkizedeki, Yule Mtawala Mkuu na Mfalme*

Habari za asubuhi, marafiki. Bila shaka nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, kwenye asubuhi hii nzuri ya kipupwe; jua likiwaka angavu; mioyo yetu ina furaha. Nilipokuwa nimeketi mle ndani na Kasisi Bw. Beeler, alipokuwa anarekodi, habari za Roho Mtakatifu kushuka juu ya jengo, nao watu wakishangilia, watoto wakifurahi. Tunashukuru kuwa hai na miongoni mwa wale ambao wanaweza kujitokeza leo katika ibada. Sasa, tunashukuru kwa ajili ya kila mmoja wenu.

2 Na jinsi mabawabu kule nyuma, mtu anapoingia, wana viti hapa, wanaweza kuketi kinyumenyume madhabahuni, na sehemu nyingine ya benchi hapa, mbele, pia, ikiwa—ikiwa watu watakuja baadaye kidogo.

3 Sasa, wiki hii ijayo tunaanza ile ziara ya mwaka sasa, ziara nyingine ya ulimwengu. Kuanzia ninii ijayo, ta—tarehe 12, hiyo ni Jumatano hii ijayo, huko Chicago, kwenye kanisa la Filadelfia na kwenye uamsho. Na halafu nadhani, kutoka hapo, sisi, asubuhi ya leo, kutoka . . . Kuanzia tarehe 3 Februari, tunaanzia huko Lubbock basi, Texas, kwenye—kwenye Ukumbi wa Cotton Bowl huko Lubbock, Texas. Kisha, kutoka hapo, hadi Phoenix. Na kisha kwa maonyesho ya mifugo kati ya Los Angeles na Lango la Kusini, huko California. Na kisha, kama Bwana akipenda, tunataka kwenda Honolulu, kutoka huko.

4 Sasa, hakika ninawathamini watu wote wanaoomba. Kama wangemwomba tu Bwana, kila siku, maombi mafupi kwa ajili ya afya ya—yangu. Mimi . . . Itakuwa vigumu kwenu kujua, upande huu wa Umilele, jinsi ninavyowategemea ninyi kuniombea ninapoondoka.

5 Nilishukuru kumsikia Ndugu Tommy, asubuhi ya leo, katika ushuhuda wake, jinsi ambavyo Mungu, huku amefungua mikono Yake, daima yuko tayari kuwapokea. Haidhuru umefanya nini, bado mikono Yake ingali imenyoshwa kumpokea kila mtu atakayemjia, haidhuru umefanya nini au hiyo dhambi ni kubwa kiasi gani. Daima yuko tayari kusamehe. Mungu akubariki, ndugu yangu mdogo.

6 Sasa, nilikuwa nikiona matokeo ya mkutano wa Jumapili iliyopita, wale watu walioombewa. Tuna mahojiano kidogo, faraghani, kuwafanya watu . . .

7 Nawaambia, mnaona, marafiki, sababu ya kutokuwa na ibada za uponyaji hapa, mnaelewa, hatuna nafasi yoyote ya kutosha kuwashughulikia watu. Hivyo ndivyo ilivyo.

Hazitangazwi kamwe, ibada za uponyaji hapa maskanini, ingawa tunawaombea wagonjwa kila wakati ninapokuwa hapa.

8 Na kumbi ni ngumu kupatikana, na kadhalika. Nanyi wageni mlio katika sehemu mbalimbali za nchi, mkiingia, hakuna watu wengi sana wa full Gospel mumu humu katika jamii au, hata hivyo, au katika viunga vya hapa. Lakini wao . . . Sio wote wanaoifadhili hii mikutano, au wanaoshirikiana katika hii mikutano, hasa, ni watu wa full Gospel, kwa sababu kuna mengi yao ambayo ni makanisa tofauti. Hatujaribu kuwakilisha shirika lolote la kanisa. Ila, tunajaribu, kwa msaada wa Mungu, kumwakilisha Bwana Yesu Kristo, na—na kuwa huru kwa wote, kila mtu.

9 Niliona tu, mimi mwenyewe, Jumapili iliyopita humu chumbani, kulikuwa na ndu—ndugu mweusi ambaye alikuwa ameokoka hivi majuzi, miezi michache iliyopita, pamoja na mke wake mpendwa. Naye mke alikuwa kiwete, hajiwezi. Naye mume ana henia ya kutisha. Basi nilipokuwa nikizungumza naye faraghani, katika ofisi ya mashemasi, kwa mahojiano ya faraghani, kwa vile alitangulia kupiga simu na kufanyiwa maandalizi. Kila Jumapili, tunao wengi tunaoweza kuwapata kila Jumapili. Ninahisi, nikiwa nimeketi pale, na uvuvio wa Roho Mtakatifu, mbona, . . .

10 Mama mmoja alikuwa ndio kwanza ameenda kule, alikuwa na magongo, ambayo yalikuwa yameninii . . . akatoka nje, akitembea bila hayo.

11 Ndipo mtu huyu, akimwamini Bwana Yesu kabisa, mbona, aliombewa, akiwa na henia kubwa ya kutisha. Ndipo nikamwambia, nikasema, "Sasa, henia hiyo itaanza, kuanzia wakati uu huu, kurudi mahali pake." Nikasema, "Sasa wakati—wakati inaporudi nyuma, basi itazame inaposinyaa, jambo ambalo litakupa imani zaidi."

12 Mnaona, imani haina budi kutegemezwa juu ya kitu fulani, si mawazo tu ya uwongo. Haina budi kuwa na kitu, kimsingi, cha kusimamia; imani huwa hivyo. Na hiyo ndiyo sababu tunaamini ya kwamba Neno la Mungu linafundisha uponyaji wa Kiungu, ukombozi wa nafsi, ukombozi wa mwili. Nasi tunaiwekea msingi juu ya Neno la Milele la Mungu.

13 Basi nikamwambia yule ndugu, "Sasa, ili uweze kujua ya kwamba nimekwambia Kweli." Maana, nikimwona mbele yangu katika maono, nilisema, "Chukua, utakapoenda nyumbani, ukaifunge kwenye hiyo henia, uzi, kisha uupime. Halafu basi uukate uzi huo, wala usiiguse tena hadi Jumapili ijayo. Na kabla hujaja huku, uchukue huo, uchukue uzi mwingine na kuuzungushia hiyo, kisha unileteе tofauti iliyopungua kwenye hizo nyuzi."

Akasema, "Nitafanya hivyo."

14 Vema, huu hapa huo uzi, yapata inchi moja na nusu imekatwa kutoka kwake, namna hiyo. Huyu hapa huyo mtu ameketi, huyo mtu, ili tu mweze kuona kile kilichotukia.

15 Sasa, jambo fulani limetukia. Sijawahi, maishani mwangu, kuona wakati wowote ambapo Mungu aliwahi kusema jambo lolote, ama kusema kwa ono au ufunuo, ila lililokuwa jinsi hasa Mungu alivyosema lingekuwa, mnaona, sawa kabisa.

16 Mkewe, Jumapili iliyopita, akija, alikuwa akitembea kwa kuegemea gongo, au kijiti, fimbo. Nami nilimwona leo. Yeye, mle ndani, asingeweza kutembea, ila kwa shida. Yeye, nilimwambia ya kwamba Bwana atamponya. Alikuwa na ki—kiungo kilichokakamaa. Nami nikamwona akipanda juu, alikuwa ameibeba fimbo yake begani mle ndani. Naye huyu hapa leo.

17 [Dada mmoja anasema, "Bwana asifiwe. Mimi ndiye yule mama."—Mh.] Yupo—yupo mama mwingine, mwingine wao kutoka huko chini . . . Nani? Huyo alikuwa . . . Alikuwa katika hali mbaya sana, akiwa na magonjwa mengi sana, Jumapili iliyopita, na ni kiwete. Naye anaishi huko chini mahali fulani karibu na Georgetown, sivyo, mama, au mahali fulani huko chini? ["Georgetown, Indiana."] Georgetown, Indiana.

Akasema, "Lakini, Ndugu Branham, mimi ni mkongwe."

18 Nikasema, "Lakini Ibrahimu alikuwa hivyo, pia, alikuwa mzee kuliko wewe, alipotakiwa kuamini jambo ambalo lilikuwa haliwezekani." Naye akaukubali, naye yule pale.

19 Na huyu hapa mama mwingine ameketi moja kwa moja nyuma ya yule mama niliyekuwa nikinena habari zake, moja kwa moja nyuma ya mumewe hapa. Huyu mama mweusi, anayeketi papa *hapa*; na yule mama mwingine, kule nyuma.

20 Zile nyuzi, kwa ajili ya ushahidi. Gongo limetoweka, kwa ajili ya ushahidi. Yesu Kristo yu hai na anatawala, kwa ushahidi mkuu kwamba alifufuka katika wafu na yuko pamoja nasi leo hii. Jinsi tunavyomshukuru kutoka kwenye vilindi vya mioyo yetu, kwamba Yeye angali hai. Hajafa. Alifufuka katika wafu, na anaishi miongoni mwa wanadamu leo, daima yu tayari, anaweza kufanya mambo mengi, kwa wingi kuliko yale tunayoweza kufanya au kuwaza. Tunamsifu kwa moyo wetu wote, kwa wema Wake kwetu.

21 Sasa angalieni kama kuna . . . Je, kuna benchi zingine humo? [Ndugu Neville anasema, "Kuna zingine kubwa huko nyuma."] Vema. Wana zingine, ambazo tungeweza kuzileta tu hapa na kuwaketisha humu jukwaani, mkipenda.

22 Sasa, kwa ajili ya somo la shule ya Jumapili, tutaninii . . . Imekuwa kura yangu, kufundisha, kidogo tu kwenye masomo ya shule ya Jumapili. Nasi, Mungu akipenda, tutajaribu kumalizia

somo ambalo tulianzisha siku chache zilizopita, hapa ka—kanisani, Jumapili chache zilizopita.

23 Na sasa, Ndugu Junior, labda, huenda ikawa wangeleta... Sijui kama ungependelea kuketi hapa jukwaani, na kuwaruhusu tu baadhi ya hao kina mama...Unaweza kuirejesha hapa, pengine, na kuifanya bo—bora kuliko vile ingekuwa, uipeleke mbele. Na mara tu darasa la shule ya Jumapili litakapoachiliwa kwenye chumba hicho, kutakuwa na viti vingine, viti vingine vitakuwa tayari.

24 Sasa, ikiwa ni mtu ambaye...labda mtu ambaye ni mshirika wa kanisa hapa. Kidogo, labda, ni aibu ama chochote kile kwa wageni kuja huku. Lakini kama mtu ni mshirika wa hili kanisa, angekuja na kuketi kwenye viti hivyo, ambalo pengine litampa mtu mwingine kiti wanapoingia.

25 Sasa, leo hii, tunajifunza katika Neno lililobarikiwa la Mungu. Kama mnakumbuka ule Ujumbe wa mwisho, ulikuwa katika Kitabu cha Waebrania.

26 Ajabu sana, kusoma Neno la Mungu! Linatupa Uzima wa Milele. Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia." Basi inapendeza jinsi gani kujua ya kwamba Yeye ametubariki, kutupa Neno lililo hai. Mungu yuko katika Neno Lake.

27 Sasa, nyote fungueni katika Biblia zenu, kwenye Waebrania mlango wa 7.

28 Nasi tutajaribu kutochukua muda mwingi sana asubuhi ya leo, bali kuinuliwa kidogo tu kwa Kristo, kwa Neno, ili tuweze kuwafanya muone kile Yeye alicho na sababu ya sisi kuwa hapa leo, kwa nini Ukristo uko vile ulivyo, kwa kunena juu ya Neno. "Nayo imani chanzo chake ni kusikia, kusikia kwa Neno la Mungu." Neno!

29 Sasa, tunaweza kuchukua kurasa na kuzirudisha nyuma namna *hii*. Lakini kuna Mmoja tu anayeweza kulifungua Neno, huyo ni Kristo. Kwa maana, walimwona katika ono, kama, "Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu," Yohana alipotazama. Wala hapakuwapo na mtu Mbinguni aliyestahili kukifungua kile Kitabu, ama angeweza, ama kuifungua Mihuri yake. Naye akamwona Mwana-Kondoo, kana kwamba alikuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Ambaye alikuja na kukitwaa hicho Kitabu katika mkono wa kulia wa Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi, na kukifungua kile Kitabu na kuifungua Mihuri.

30 Sasa, Yeye ndiye Mwandishi wa Kitabu hiki. Hebu tuzungumze naye kwa muda kidogo tu kabla hatujaingia kwenye Kitabu.

31 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, kwa mioyo mikuu ya upendo mkuu tunakuja leo kutoa shukrani zetu na sifa na kulitukuza Jina Lako tukufu. Kwa kutujali sana, "Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa badala yetu, asiye na hatia kwa ajili ya wenye hatia. Akijitwika dhambi zetu zote, akiziondoa," na kulipa bei iliyo kuu; akamridhisha Mungu. "Kisha akafufuka tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, ameketi mkono Wake wa kuume leo hii, yu hai sikuzote ili kutuombea tunapoungama." Loo jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya tumaini hili thabiti tulilo nalo! Wakati yote yanayotuzunguka yanaporomoka, hata maisha ya kibinadamu yenyewe, mioyo yetu inaelekezwa kwenye tumaini hilo la Milele, lenye baraka.

32 Wengi hapa ni wahitaji, asubuhi ya leo, Baba, kwa ajili ya roho zao, kwa ajili ya nafsi zao. Tunaomba kwamba utawaokoa wasiookolewa. Tujalie, Bwana. Wape matembezi ya karibu wale ambao hawakujali. Nasi tunaomba ya kwamba utawaponya wote walio wagonjwa, ili litimie lile lililonenwa na Bwana wetu Mwenyewe, "Mambo haya nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya." Na kwamba Yeye alisema kwamba hatuna budi "Kwenda ulimwenguni mwote na kuihubiri Injili; tuweke mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

33 Na kuona hapa katika jengo hili dogo, asubuhi ya leo, watu wengi ambao walikuwa kwenye magongo siku chache zilizopita, wakitembea leo bila hayo, kawaida. Wakiinuliwa na kushikiliwa juu kwa kuzingirwa kwa mikono ya milele ya Bwana wetu Yesu Kristo, wakitembea! Wale waliokuwa wakifa kwa kansa, wako hapa, wazima. Watumishi wako, madaktari, wakitoa taarifa, hawawezi kuipata tena. Imekwisha. Tunakushukuru kwa mambo haya.

34 Utusamehe kupungukiwa kwetu, na uijaze mioyo yetu na upendo. Nena nasi kupitia Neno Lako sasa, kwa maana tunaomba katika Jina Lake. Amina.

35 Utangulizi mdogo tu wa awali, tupate mawazo ya somo letu la Maandiko asubuhi ya leo. Ni, tumekuwa tukizungumza juu ya hakikisho la tumaini lililo ndani yetu, lililotolewa vizuri sana hapa katika waraka wa Waebrania. Baada ya kusoma jinsi Mungu alivyoshughulika na watu Wake, Israeli, katika siku zilizopita, ndipo tunaona kwamba hiyo ahadi ililetwa kwetu pia, inatupa hakikisho kubwa tunapoona kwamba mambo hayo yote yaliyotukia huko nyuma katika siku hizo yalikuwa mifano ya kile ambacho Mungu anatufanyia siku hizi, kwa watoto Wake waaminio.

36 Na sasa utangulizi mdogo tu wa awali wa somo la Jumapili iliyopita, la mlango wa 6 wa Waebrania. Tutaanzia yapata kifungu cha 12, ama cha 13 hapa.

*Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sababu alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapia, aliapa kwa nafsi yake,*

37 Nina hakika darasa linaweza kukumbuka jinsi tulivyochukua jambo hilo, kuona kile Mungu alikuwa amefanya, jinsi alivyokuwa amemwahidi Ibrahimu ya kwamba angempa agano hili, na kulifanya pamoja naye na Uzao wake, milele baadaye.

38 Naye Mungu akaapa kwa kiapo. Basi yeyote anayeapa kwa kiapo huapa kwa aliye mkubwa kuliko wao. Kwa hiyo, Mungu alikuwa hana mkubwa kuliko Yeye, Mwenyewe, wa kumwapia, hivyo basi akaapa kwa nafsi Yake kwamba atalitimiza agano hili kwa Ibrahimu. Basi, ni msingi imara jinsi gani, enyi watakatifu wa Bwana!

39 Ikiwa tutalikaribia somo hili leo, kwa busara kabisa, kwa utulivu, kamwe tusisisimkwe. Imani haisisimkwi kamwe. Imani haijiharakishi. Imani inajua inachozungumzia.

40 Hujawahi kuona Bwana wetu akisisimkwa na chochote. Akiwa amesimama kando ya kaburi la mtu aliyekufa, Yeye alikuwa mtulivu tu kadiri alivyokuwa alipoketi juu ya ule mlima na kuutazama Yerusalemu.

41 Wakiwa wamesimama juu ya taabu, juu ya chombo katika bahari iliyochafuka, na mawimbi yakisukasuka, alikuwa amestarehe kabisa ndani ya Mungu, hata hakuyazingatia hata kidogo kiasi cha kuamka. Daima haisumbuki, imani.

42 Sasa, tunaona hapa ya kwamba sababu tunaweza kuwa tusiosumbuka, ni kwa kuwa ilipewa baba yetu Ibrahimu na watoto wake. Naye Mungu, Yeye aliyetoa ahadi, aliapa kwa kiapo kwamba ataithibitisha na kuitimiza. Naye amefanya hivyo.

43 Nasi tunaona, wana wa Ibrahimu si Wayahudi kwa nje, ambalo lilikuwa kabila la . . . kutoka katika ukoo wa Ibrahimu. Lakini, kupitia Ibrahimu alikuja Isaka; kupitia Isaka akaja Kristo; kwa njia ya Kristo, ulimwengu ukabarikiwa. Maana ilisema, "Kwa Ibrahimu na kwa Uzao Wake, ambao ulikuwa ni Kristo." Na kupitia hapo, kwamba, makabila yote ya dunia yaliingizwa katika agano hili.

44 Nalo agano lilipewa Ibrahimu bila masharti. Sio, "Ibrahimu, ikiwa utafanya jambo fulani, nitafanya *hivi*." Lakini, "Tayari nimelifanya." Mnaona?

45 Si kile tufanyacho; ni kile ambacho ametufanyia Yeye. Hakuna kitu tunachoweza kufanya ili kustahili chochote. Tungewezaje, sisi tusio haki, kufanya lolote la kustahili jambo fulani mbele za Yehova Mungu mkuu, na utakatifu Wake mkuu sana? Mnaona? Sisi, jambo pekee tunaloweza kufanya ni

kukubali na kushukuru kwa yale ambayo tayari ametufanyia Yeye. Loo, ni rahisi sana. Sivyo?

46 Nami nina hakika ya kwamba mara nyingi, katika mawazo ya watu, kwamba wanajaribu kufanya uponyaji wa Kiungu, na kadhalika, kitu kikubwa cha kufikia, kitu kilicho mbali sana, "Laiti ningaliweza kukifikia!"

47 Unaweza kuwazia Yesu akisema, "Sasa hebu niichunguze imani Yangu nione kama nina imani ya kutosha kufanya hili. Nione kama itanibidi kufunga kwa muda kidogo, kuona kama nitakuwa na imani ya kutosha kufanya jambo hili"? Alikuwa kabisa hawazii imani aliyokuwa nayo. Yeye alinena tu, na alijua ya kwamba ingekuwa hivyo.

48 Kama vile mumetoka kwenye makazi yenu leo hii. Labda mnataka kurudi kwenye makazi yenu. Ulimwambia mke wako, au wapendwa wako, "Nitarudi, muda fulani baada ya adhuhuri." Unajuaje kuwa utarudi? Hujaribu kujiuliza, "Je, nina imani ya kutosha kwenda nyumbani? Je, nina imani ya kutosha kuendesha gari langu?" Unauzungusha ufunguo wako bila kuwazia, unaliendesha gari, na kwenda nyumbani. Unaona? Ni imani isiyo na ufahamu inayofanya hivyo.

49 Hivyo ndivyo ilivyo katika Kristo. Tunasema tu bila kufikiria, "Hilo ni Neno Lake. Hilo latosha. Hamna lingine," na kuendelea. Hivyo ndivyo wanavyopona.

Sasa, "Mungu akiapa kwa nafsi Yake, hakuna mkuu zaidi."

50 Tutaharakisha na kuliingilia, kwa maana somo letu la leo ni juu ya Melkizedeki: *Melkizedeki, Yule Mtawala Mkuu Na Mfalme*.

51 Sasa mlango wa 14 unasema:

> *Akisema, Hakika yangu* kubariki *nitakubariki, na kuongeza nitakuongeza.*

52 Maana, Yeye alipaswa kuongezwa kwa kila taifa. Na Injili, kwa njia ya Kristo . . . Sasa, isingewezekana chini ya majira ya torati, kwa sababu haikufikia umbali huo; ni kwa waliotahiriwa pekee, na huyo alikuwa ni Myahudi. Lakini katika milki ya Roho Mtakatifu, Yeye ameutahiri kila moyo, mnaona, mataifa yote. Angemwongezea Ibrahimu kwa mataifa yote.

> *Na hivyo, kwa kuvumilia akaipata ile ahadi.*

53 Jinsi tulivyokaa juu ya hilo, jinsi, "Ibrahimu, akivumilia kwa subira." *Kuvumilia, ni* kumwona (nini?) Mungu asiyeonekana kana kwamba anaonekana, amesimama mbele yake. "Na baada ya kuvumilia, baada ya kuvumilia hivyo vita vikali, akairithi ile ahadi."

54 Sasa si ni ajabu? Inaonekana kama Mungu angeweza tu kumfikia na kumpa ile ahadi papo hapo, na kuifanya hiyo kazi papo hapo. Angeweza kuifanya.

55 Hana, alipokuwa hekaluni, naye alikuwa akiomba. Basi Eli alitoka nje, akafikiri alikuwa amelewa. Ndipo akasema, “Mimi si mlevi, lakini ninaomba kwamba Mungu ataiondolea aibu yangu.”

Akasema, “Bwana Mungu na akujalie ha—haja yako.”

56 Sasa, Mungu angeweza kumweka mtoto Samweli moja kwa moja mikononi mwa Hana. Sisi sote tunajua hilo. Yeye ni Muumba wa vitu vyote, hunena tu vikawa. Angeweza kumweka moja kwa moja mikononi mwa Hana. Lakini, badala ya kufanya hivyo, ilikuwa utaratibu wa kawaida wa miezi tisa kabla ya mtoto huyo mchanga kuwasili. Angeweza kuifanya hivyo mara moja, lakini hakulifanya mara moja. Alimpa tu ahadi. Naye akairithi hiyo ahadi.

57 Wakati Mungu alipomwambia Musa, alipoanza kutoka, kwenda katika nchi ya ahadi, “Ahadi hiyo yote,” alisema, “Nilimpa Ibrahimu miaka kadhaa iliyopita, imezingirwa kote na Wafilisti na kila namna ya watu wakuu huko, mashujaa.” Akasema, “Sasa yote ni yako.” Kulikuwa na Waamori, na Wahivi, na Waperizi, na hao wote huko, na Wahivi, Wayubini, Wafilisti, kila kitu katika Palestina. Sasa Mungu akasema, “Nimekupa wewe. Ni yako. Sasa nenda ukaimiliki.”

58 Loo, natumaini mnaliona, enyi watu. Ni jambo ambalo ninataka kuwaletea, kuweka imani yenu mahali panapostahili. Watu wengi, kama ninavyoona, wanaweza . . . Wanayo imani, laiti wangejua jinsi ya kuiweka itende kazi.

59 Wakati Benjamin Franklin alipoupata umeme kwa mara ya kwanza, alisema, “Nimeupata. Nimeupata.” Lakini hakujua alichokuwa nacho.

60 Moja kwa moja akaja Thomas Edison, na kusema, “Itatufanyia kazi.” Wala hakujali ilichukua muda gani; alijaribu nyaya elfu kumi. Lakini, hata hivyo, alipata waya ambao hatimaye ungebeba elektroniki, au umeme, katika waya. Alijua ilikuwa ni nguvu fulani, nazo nguvu hizo zingefanya kazi kwa manufaa yetu.

61 Na sasa tulipata wokovu, utakaotuokoa na dhambi; ambao utamchukua mwanamke ama mwanamume aliye mwovu sana, mlevi, kahaba, na kuwafanya mtoto wa Mungu. Vema, imani iyo hiyo . . . Nguvu zizo hizo zitakazomwinua mwanamume au mwanamke aliyepungukiwa nayo, zitafanya kazi kwetu kwa njia nyingi mbalimbali. Itaponya miili yetu, ikiwa unaweza tu kupata njia sahihi ya kuiendea. Huna budi kupata njia ya kufanya hivyo.

62 Kama vile, iwapo ningekuwa na sha—shamba juu ya kilima *hiki*, lililojaa mahindi mazuri, nayo karibu yanyauke kwa ukosefu wa maji. Nami nikapata kisima cha chemchemi upande *huu* wa kilima. Vema, siwezi kukifanya hicho kisima cha maji kutupa maji *hapa* chini, na juu upande huu wa kilima, kulimwagilia maji. Lakini sina budi kuchunguza shamba hilo

nipate kujua jinsi maji hayo yatachukua mkondo na mwendo wake, na kuja karibu na kumwagilia mazao hayo. Yatafanya hivyo ikiwa nitayaacha yafuate njia yake.

63 Na hicho ndicho kitu kile kile alicho Roho Mtakatifu, na ahadi ya Mungu. Kama tu tutamwacha apitie njia Yake; na sio sisi kuingilia kati, si sisi kutupa mashaka yetu pale, maana *hili* halikufanya na *lile* halikufanya. Mwache tu Roho Mtakatifu wa Mungu afanye kazi, nawe utulie juu ya ahadi, atafanya kile hasa Mungu alisema atafanya.

64 Ibrahimu alikuwa mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, Mungu alipomtokea kwa jina la Mwenyezi Mungu. Hilo "Mwenyezi," hapo, linatokana na neno la Kiebrania la *El Shadai,* ambalo linamaanisha "kifua, au titi la mwanamke." Sasa alikuwa ni mzee. Nguvu zake zilikuwa zimeisha. Lakini *El Shadai ni* Mwenyezi, "mpaji nguvu." Na yote Ibrahimu aliyopaswa kufanya kupata ahadi hii, ilikuwa ni kudumu moja kwa moja juu ya ahadi hiyo. Kwa maneno mengine, ni kama mtoto kwa mama yake; na kunyonya kutoka kwa mama, nguvu kwa ajili ya huyo mtoto.

65 Nasi tunafanya jambo lile lile tunapomjia Mungu na kuona ahadi Yake. Tunalala moja kwa moja Kwake na kutoa kwenye Neno Lake, nguvu za Mungu, zinazotolewa katika mwendo Wake, sio kuchukua mawazo yetu wenyewe; kuliamini tu.

66 "Baada ya kuvumilia, alipata ile ahadi." Loo, ninapenda tu hilo! Sasa, jambo lile lile linalofanya kazi kwa wokovu, vivyo hivyo linafanya kazi kwa uponyaji wa Kiungu. Jinsi Mungu, katika upendo Wake mkuu na rehema isiyo na kikomo, anavyotupa sisi! Sasa:

> *Akisema, Hakika . . . nitakubariki, na . . . nitakuongeza.*
>
> *Na hivyo, akiisha kuvumilia kwa subira,* aliivumilia *ile ahadi.*

67 Kifungu cha 16:

> *Kwa maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, na kiapo ni uthibitisho,* kuyathibitisha, *kwao* ni *ukomo wa ushindano wote.*

68 Kwa maneno mengine, kiapo kikiapwa, basi hicho ndicho kikomo cha mambo yote. Ukija na kusema, "Ndugu Branham, mimi, kama Mkristo, ninaweka mkono wangu juu ya Biblia na kuapa kwa uchaji kwamba nitafanya jambo fulani. Mungu akinijalia kuishi kufanya jambo hilo, nitalifanya." Vema. Ndipo, kwangu mimi, hicho ndicho kikomo cha mashaka yote. Mnaona? Umeapa kwangu kwamba utafanya hivyo.

69 Naye Mungu alimwapia Ibrahimu kwamba angetimiza agano hili pamoja naye na wa Uzao wake milele. Mungu aliapa

kwa nafsi Yake, ya kwamba angefanya hivyo. Na kwa kufanya hivyo. . .

70 Chini ya torati ya kale, ulipokula kiapo chini ya torati ya kale, ulimchinja mnyama, ukamkata vipande viwili. Ndipo wale watu wawili waliokula hicho kiapo, walisimama kati ya yule mnyama, nao wakaandika kwenye kipande cha karatasi mkataba fulani. Ndipo kipande hicho cha karatasi kikapasuliwa, na kupewa huyo mmoja na huyo mtu mwingine. Kisha wakala kiapo juu ya mnyama huyu aliyekufa, kwamba, kama watalivunja agano hilo kati yao, na wawe kama mnyama huyu aliyekufa.

71 Basi, Mungu, kwa kuwa hana mwingine wa kumwapia, aliapa kwa nafsi Yake, Naye akala kiapo juu ya mwili wa Bwana Yesu Kristo, akiuona katika kivuli. Na katika hilo agano, wakati alipompeleka Kristo Kalvari, aliutenganisha mwili na nafsi Yake. Ndipo akauinua mwili Wake, aketi mkono Wake wa kuume; kisha akamrudisha Roho Mtakatifu, apate kuwa ndani ya Mkristo, kufanya jambo lile lile hapa Kanisani alilofanya katika Kristo alipokuwa hapa duniani. Na kuthibitisha, kwa jambo hilo, ya kwamba atatufufua katika siku za mwisho, kuketi pamoja Naye na kuwa pamoja Naye katika Ufalme Wake.

72 Na, leo hii, kumwona Roho Mtakatifu yeye yule, aliyekuwa juu ya Yesu Kristo, akitenda kazi Kanisani, akithibitisha kila kitu ambacho Mungu alisema! Ni tumaini la ajabu jinsi gani linalojengeka ndani yetu, kuwazia ya kwamba sisi ni watoto Wake, na tumebarikiwa na Uwepo Wake! Na sasa Yeye yuko hapa pamoja nasi, kama thibitisho lisiloweza kukosea ya kwamba Yeye ni Bwana Mungu Yule aliyempa Ibrahimu ile ahadi.

73 Sasa sikilizeni, kifungu cha 17.

> *Katika neno hilo Mungu akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithi wa ile ahadi jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati:*
>
> *Ili kwa vitu visivyoweza kubadilika,*. . . ambapo *Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yaliyowekwa mbele yetu:*

74 Ni ahadi ya ajabu jinsi gani, "Vitu viwili visivyoweza kubadilika!" Mungu hawezi kusema uongo, na awe Mungu. Sasa, kama Mungu ametoa ahadi katika Biblia Yake hapa, tunaamini Biblia kuwa ni Neno la Mungu lisiloweza kukosea. Na ikiwa Mungu ametoa ahadi katika Biblia hii, tunayo faraja hii na tunajua kwamba Mungu hawezi kusema uongo. Kwa hiyo, tunapoona Yeye aliliahidi katika Biblia, tunaliamini, nafsi, mwili na roho. Hawezi kusema uongo. Sasa kama kuna kosa lolote, liko ndani yetu, si katika Mungu. Kwa maana, Mungu

anawajibika kwa Neno Lake, kwa maana ameapa kwa Neno Lake. Loo, jamani!

75 Nina hakika, tunapofikia kuliona kwa mwanga huo, mambo huanza kujipanga na kulundikana tofauti na ilivyokuwa zamani. Uponyaji wa mwili hauwi hadithi ya uongo. Unakuwa ukweli. Ubatizo wa Roho Mtakatifu hauwi kitu cha muhemko, cha kujihamasisha. Unakuwa halisi, wa Uwepo wa Bwana Yesu Kristo unaokaa ndani, kubadilisha maisha.

76 Siku chache zilizopita usiku, katika mkutano wa maombi, mtu mmoja aliniambia, "Roho Mtakatifu hakutolewa. . . Ila tu kwa wale kumi, au wale kumi na wawili, kwenye Siku ya Pentekoste."

77 Nikasema, "Vema, basi, vipi kuhusu wale mia na ishirini waliokuwa pale wakati ule ule, walioupokea? Vipi hata kule chini kwenye nyumba ya Kornelio, wakati Mataifa walipoupokea? Miaka thelathini na mitatu baadaye, wakati Paulo alipowauliza wa—wale Wabaptisti kama walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu tangu walipoamini; naye akaweka mikono yake juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Akiliweka kanisa la Korintho katika utaratibu, 'Pia aliweka katika Kanisa, mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, karama za uponyaji,' na karama hizo zote za ajabu, miaka na miaka baada ya Pentekoste."

78 Basi, ndivyo ilivyo leo hii, kwa kila mwaminio. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Umbali gani? "Ulimwenguni kote." Wangapi? "Watu wote." "Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu watatoa pepo, na kuwaponya wagonjwa, na kadhalika."

79 Haya basi. Ni ahadi ya Mungu, ambayo aliapa ataifanya. Haijalishi ni kiasi gani kinachoinuka kujaribu kubuni au kuiiga, ni vitu vingapi vinavyoinuka kujaribu kuipinga ama kuiangusha, itaendelea mbele zaidi na zaidi, milele, kwa maana Mungu ameapa kwa nafsi Yake kwamba ataitimiza. Kama nikishindwa kulihubiri, na kuliaibisha, Mungu atamwinua mtu mwingine mahali pangu apate kuendelea Nalo. Ukishindwa kuliamini, kutakuwa na mtu atakayeingia mahali pako, kuliamini, badala yako, kwa maana Mungu ameapa atafanya hivyo. Loo, ni faraja ilioje hilo linatupa!

80 Na sehemu nzuri kuhusu jambo hilo, rafiki yangu Mkristo, ni kuwazia, ya kwamba sasa tunao ushahidi Wake. Tunao hapa katika baraka. Tunao katika nguvu. Tunao katika miujiza. Tunao katika ishara. Tunao katika picha. Tunao katika kila njia ambayo Mungu ameiahidi, hata zaidi ya vile Yeye alivyoahidi kutupa sisi. Nao ni Ukweli usioweza kukosea. Ukweli, si wa mwanadamu, si ukweli wa mwalimu fulani au mwanafalsafa,

lakini ni Ukweli wa Mwenyezi Mungu. Nalo linatupa tumaini la jinsi gani! Si ajabu tunaweza kuimba:

> Tumaini langu halijajengwa juu ya chochote pungufu
> Ila Damu ya Yesu, pamoja na haki;
> Wakati yote yaliyoizunguka nafsi yangu yanapotoweka,
> Basi Yeye ndiye tumaini na nanga yangu.
>
> Kwa maana, juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, tunasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

81 Iwe ni umaarufu, iwe ni kanisa letu, iwe ni marafiki zetu, washirika wetu, hata iwe ni nani; iwe ni daktari wetu, iwe ni kuhani wetu, iwe ni mhubiri wetu; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao. Kristo, peke yake! Na kila mtu ambaye amewahi kuwa kitu chochote katika uwanja huu mkubwa wa vita wa ugomvi, wamekuwa wanaume na wanawake ambao walisimama peke yao juu ya hayo masadikisho. Wakati kila kitu kingine kilishindwa na kuanguka karibu nao, bado walisimama.

82 Abraham Lincoln, wa kale, alishawishika kwamba alikuwa sahihi. Alisimama peke yake, kwenye imani zake, lakini aliithibitisha na kutia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake mwenyewe.

83 Yesu Kristo alisimama peke yake, katika siku Yake, kama mfano kwamba kila mtu, juu ya usadikisho wake wa Kweli ya Milele ya Mungu, ambaye atachukua msimamo wake, na kusimama, atasimama peke yake. Bali, si peke yake; pamoja na Mungu! Mwenzetu asiyeonekana anayetufuata katika safari ya maisha, kote katika vivuli, vya mabonde ya uvuli wa mauti, na kuingia Umilele. Bado atakwenda pamoja nasi, na awe Mungu.

84 Basi matumaini yetu yamejengwa juu ya nini asubuhi ya leo? Maana, Mungu aliapa ya kwamba angemfanyia hivyo Ibrahimu. Aliapa si kwa Ibrahimu pekee, bali kila mmoja wa Uzao wake. Uzao ni nani? Ni . . . Ninyi ambao mmepata mwaliko wa kuja kwa Bwana Yesu Kristo, Uzao wa Ibrahimu. Bila shaka, kunao watu ambao hawajaitwa. Lakini, kwa kila mmoja wenu hapa asubuhi ya leo, ambaye amepata wito.

85 Kwa nini uko hapa kanisani asubuhi ya leo? Kitu fulani kilikwambia uje. Unajua haikuwa ni adui, kujaribu kukufanya utende mabaya; kujaribu kukufanya utende mabaya, uje kanisani. Hungeweza kufanya hivyo. Unapokuja kanisani, unatenda vema.

86 Naye Yesu alisema, kwa Maneno Yake Mwenyewe, ya kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote watakaokuja, nitawapa Uzima usio na mwisho, na kumfufua katika siku za mwisho." Wazieni hilo, kwamba kila mtu ajaye kwa mwaliko wa Bwana Yesu Kristo,

ameahidiwa Uzima wa Milele na ufufuo katika siku za mwisho; na Yehova Mungu Ambaye aliapa kwa kiapo ya kwamba angefanya jambo hilo, na kumtuma Mwanawe na kulithibitisha Neno. Naye akaapa atafanya hivyo; akalitoa kama mfano, kwa Ibrahimu; akalitimiza katika Yesu Kristo, akamfufua!

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
> Siku moja yuaja—loo, siku yenye utukufu!

87 Haya basi. Kuhesabiwa haki kwetu! Kila mara unaposikia madonge yakianguka juu ya jeneza; wakisema, "Majivu kwa majivu, na vumbi kwa vumbi, udongo kwa udongo," imani yetu inaangalia mbali katika nchi nyingine huko ng'ambo, ambako kuna kaburi tupu; kwamba, siku moja tukufu, Yeye aliyeahidi kuja, atakuja. Na kwa hakika kama vile Yesu alivyofufuka katika wafu, tutafufuka pamoja Naye katika ufufuo. Ni tumaini zuri jinsi gani tulilo nalo!

88 Sasa, moja kwa moja chini, upesi. Muda wetu utatuacha kabla hatujajua. Sasa, ninaamini ni kifungu cha 19.

> *Tuliyo nayo kama nanga ya nafsi, yenye salama na yenye nguvu*. . .yaliyoingia *hata mle* mlimo ndani *ya pazia;*

89 Nanga ya nafsi yetu, iliyoingia ndani ya pazia, ng'ambo ya pazia, na kutia nanga!

90 Unajua, meli, wakati mwingine. . . Watumishi na kadhalika, wanajua, nanyi ambao mmekuwa baharini. Wakati, kwa kweli, mawimbi yanapoanza kuipiga mashua kwa nguvu sana, wao huitia nanga. Nayo ina kamba inayoshushwa, inayoishikilia. Nayo inaweza kuirusha *hivi*, na kuzunguka *vile*, lakini nanga hiyo inaishikilia. Nanga! Hawawezi kuona ardhi, popote. Lakini wanaangusha nanga ng'ambo ya pazia, ambayo ni maji, nayo nanga hiyo inashuka hadi chini ya bahari, juu—juu ya mlima fulani mkubwa mahali fulani. Nayo inakokotwa mpaka inashikiza kwenye mlima huo, inashikilia kwenye mwanya ule pale, wala bahari yote haiwezi kuisogeza tena. Imetiwa nanga, haionekani.

91 Na kila mtu ambaye amempokea Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi, amezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, umetia nanga. Ikiwa wewe ni mgonjwa, na tumaini lako limejengwa juu ya Kristo, umetia nanga yako. Daktari anaweza kusema *hivi, vile*, ama *vinginevyo;* lakini, maadamu imani yako inatazama kule! Mawimbi, vipindi vya ugonjwa, homa inaweza kuibuka, na kila kitu namna hiyo, lakini nanga yako inashikilia ndani ya pazia.

92 Mahali fulani huko ng'ambo katika nchi ya kufikirika, aisee, "Je, matumaini yako yamejengwa juu ya nini? Daktari alisema imekwisha. Dawa inasema haiwezi kufanya chochote. Upasuaji

umeshindwa." Lakini matumaini yangu hayajajengwa katika hayo.

93 Tuna tumaini letu ndani ya pazia. Pazia gani? Kupitia kumwagwa kwa Damu Yake, ambayo ilitenganisha Roho Wake na mwili Wake. Na, katikati ya pazia hilo pale, nanga imeshika kitu Fulani.

94 Niliona meli, wakati mmoja, iliporushwarushwa huko nje. Nami nikawazia, "Ni kitu gani kinachoshikilia meli hiyo katika sehemu iyo hiyo?" Sikuweza kuelewa. "Imeketi kule baharini?" Nami nikaona mawimbi yangeipeleka *huku*, na kurudi nyuma *huku*, wala haikusogea kutoka mahali hapo. Singeweza kuona chochote. Lakini kulikuwa na waya mdogo, kamba, iliyoshuka kutoka kwenye gubeti la meli hiyo, hadi kwenye nanga ambayo ilikuwa imeshika kitu chini ya ninii yangu. . . ambapo nisingeweza kuona, ng'ambo ya hayo maji. Nayo ilikuwa imeshikilia hapo. Ndipo nikasema, "Mungu asifiwe!"

95 Naam, siku moja, nilipata nanga. Nikasoma hapa chini, ilisema, "Atakaye, na aje." Nilitupa nanga hiyo ng'ambo ya kitu ambacho nisingeweza kuona. Kitu fulani kikashikilia. Na wakati vita vimepamba moto, hiyo Nanga hushikilia ndani ya pazia. Wakati makafiri wanapoinuka, na matatizo yanapotokea, na yote yanayonizunguka yakishindwa, nanga yetu inashikilia ndani ya pazia. Iko wapi? Sijui. Lakini iko ng'ambo ya pazia, mahali fulani kule, imetiwa nanga kwenye Mwamba wa Miaka. "Nanga yetu ni salama, haitikisiki. Inashikilia ndani, ndani ya pazia."

*Tuliyo nayo kama nanga ya nafsi, yenye salama na yenye nguvu, . . .*

96 "Yenye salama na yenye nguvu." Loo, laiti tungelikuwa na wakati mwingine zaidi, kupata kile ambacho *hakikisho* linamaanisha. "Uhakika," kitu ambacho unajua, na hakikisho lako. Hakikisho ni nini? "Mungu aliapa kwa kiapo atafanya hivyo." Hilo ndilo hakikisho.

97 Hapa wakati fulani uliopita, mtu alinijia, naye akasema, "Billy, ninataka kukuuzia hati ya bima."

98 Sasa, bima ni sawa. Sina yoyote, mimi mwenyewe. Nadhani nilikiuka mipaka kuihusu. Ka—kampuni moja ilimhadaa maskini mzee baba yangu, wakati mmoja, kwa nyingi, kwa sababu alikuwa asiye na elimu kabisa kusoma hiyo hati. Naye wakili wa Filadelfia asingeweza kusoma moja vizuri, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo akasema. . . Akamwuzia hati hii. Naye akailipia, kwa ajili yangu na ya ndugu yangu, kwa muda wa miaka ishirini. Akaja, akasema, "Itakuwa na thamani ya dola mia tano mwisho wa kipindi chake." Na kupitia kule kuzorota kwa uchumi na kadhalika, maskini huyo jamaa mzee akifanya kazi! Mwishowe, walituambia walikuwa wameisoma hiyo hati

vibaya. "Ilikuwa na thamani ya dola saba na senti hamsini." Kwa hiyo, kidogo ilinitia uchungu. Sasa, zote haziko hivyo. Kunao mawakala wa bima wameketi papa hapa sasa.

99 Mara nyingi, watu wamekuja na kusema, "Billy, ninataka kukuuzia bima." Sasa, nadhani ni sawa kabisa.

Nikasema, "Angalia, nina bima."

100 Naye akasema, "Je, una bima ya aina gani?" Kasema, "Una hati gani?"

Nilisema, "Uzima wa Milele."

Akasema, "Ati Uzima wa Milele?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Kasema, "Ni nani anayeuza hizo hati?"

Nikasema, "Bwana Yesu."

Akasema, "Ati una bima?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Kasema, "Ni ya aina gani, kweli? Ni nini, Billy?"

Nikasema, "Ni bima."

Akasema, "Ati nini?"

101 Nikasema, "Hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni wangu! Ee ni mwonjo ulioje wa utukufu wa Kiungu!"

102 Akanikumbatia; rafiki wa ujanani. Tulikuwa tumesimama moja kwa moja ng'ambo ya barabara hapa. Akasema, "Billy, hiyo haitakuweka makaburini hapa juu."

103 Nikasema, "Najua. Lakini itanitoa. Sina wasiwasi juu ya kuingia humo. Lakini itanitoa huko." Hiyo ni kweli.

104 Ningeweza kuwazia juu ya bima yangu nilipokuwa mgonjwa, lakini haikunisaidia chochote. Lakini, bima yangu, ya Yesu, nilikuwa na nanga, "salama," lile hakikisho kwamba, "Mungu aliapa kwa nafsi Yake," angetimiza kila Neno aliloahidi.

105 Mayo waliposema, "Hakuna tumaini kwako," hakuna tumaini kwangu kuishi; nilikuwa na kichefuchefu ambacho hatimaye kingeniua. Lakini nanga yangu ikashikilia ndani ya pazia. "Vema, unaona nini?" Sijui ninachokiona. Kuna kitu nijuacho.

106 Ndivyo ilivyo. Unakijua. Si kwa matendo. Ni kwa imani. Tunakiamini.

107 Ibrahimu alikuwa na hakikisho la aina gani kutoka kwa daktari, shirika la matibabu la Ur-i, au popote pale? Alipokuwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara tisini, walikuwa wamzae mtoto. Lakini nanga yake ikashikilia ndani ya pazia, kwa maana Mungu alimpa ahadi naye akatulia juu yake. "Na kuviita vitu visivyokuwako kana kwamba vilikuwako," kwa sababu akijua

ya kuwa Mungu aliweza; hili hapa, Mungu aliweza kufanya kile alichokuwa ameahidi.

108 Aliumba ulimwengu. Aliniumba mimi. Aliumba kila kitu. Alikuumba wewe. Alivifanya vyote, kila kitu, kwa Neno Lake. Nalo Neno Lake litafanya kile hasa linalosema Yeye, litafanya.

109 Sasa, loo, vipi, tumaini lililoje! "Tumaini ambalo tunalo, hakikisho la tumaini, ndani ya pazia."

110 Itabidi tuharakishe sasa kwa sababu tuna safu kubwa ya maombi inayokuja.

111 Angalieni, "Ambapo . . . " Loo, jamani! Vema, tazameni, kila mtu sasa. Kifungu cha 20, angalieni tu jambo hili.

> *Alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu* aliingia, . . .

112 Mtangulizi wa nini? Mtangulizi wa wokovu wetu, kimwili na kiroho. "Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Mtangulizi wa wokovu wetu tayari ameingia. "Hakikisho, tayari limeingia, ambalo ni Yesu."

> . . . *amefanywa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.*

113 Sasa tunafikia ambapo tunataka kupata somo hili upesi sana sasa na kuliingilia.

114 Ahadi hizi zote kuu, tunazijumuisha kuwa kitu kimoja, kwamba, "Yesu, mtangulizi wetu, Ambaye alikuwa Mzao wa Ibrahimu," kwa njia ya Roho Mtakatifu ametuita kwenye tumaini hili lenye baraka tulilo nalo sasa, "nanga ya nafsi, salama na imara, iliyotiwa nanga ndani ya pazia." Yesu huyu, akifanyika mtangulizi, ambaye alikuwa katika mfano wa Melkizedeki.

115 Sasa, Mtu huyu mkuu, Melkizedeki, tunataka kuongea juu Yake kwa dakika chache zijazo. Tukiharakisha, dakika kumi au kumi na tano zijazo.

116 Na halafu, kwa ajili ya mstari wa maombi, jenga imani yako sasa. Usimruhusu ibilisi akunyang'anye chochote. Uko hapa asubuhi ya leo, katika jengo hili dogo, ambapo Mwenyezi Mungu atakuja katika makao haya duni hapa. Unasema, "Yanaonekana mabaya sana." Lakini alikuja kwenye hori.

117 Atakuja kwenye moyo wowote mnyenyekevu ambao utafunguka na kusema, "Naam, Bwana Yesu, ninaamini Hilo. Huenda hata nisilielewe, lakini ninaliamini, kwa vyovyote vile."

118 Tumaini hili lenye baraka tulilo nalo, "Kristo, mtangulizi, amekwisha kuja." Mnajua mtangulizi ni nini? Kitu kinachotangulia, au kinachoenda mbele. Kristo, akiwa

mtangulizi, basi, wa wokovu wetu, alikuja duniani; na kuwa kielelezo cha Kanisa, kwamba Kanisa lilipaswa kumaliza kazi Zake, au kuendeleza kazi Zake, akiisha kumaliza dhabihu Yake pale Kalvari. Mnaliona? Angalieni.

119 Ndipo, Yeye alizaliwa katika unyenyekevu, papo hapo horini. Alidhihakiwa; kama vile unavyoweza kudhihakiwa wewe, au mtu mwingine yeyote anayemtumikia. Lakini wakati akiwa duniani, Yeye, "Ambaye hakuwa na upendeleo," aliwapenda wote. Yeye, aliwaponya wote. Aliwabariki wote. Alifanya mema popote alipoenda. Aliyatoa maisha Yake kama dhabihu; akafa, akazikwa. Akafufuka, akapaa juu, kama mtangulizi kwetu.

120 Naye Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake amerudi kuwa pamoja na Kanisa, kuliongoza na kulielekeza. Akizungumza, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Lakini, ninyi mtaniona, kwa maana Mimi. . . " "Mimi" ni kiwakilishi nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Kama, tukielekeza akili zetu kwenye dhabihu Yake iliyo kuu sana, kama mtangulizi wa tumaini letu lenye baraka tulilo nalo ndani ya pazia sasa.

121 Basi, kwa imani tunaliamini. Nanga yetu inaenda kule, na ncha Zake, katika Neno la Mungu, zinashikilia ndani ya pazia. Na, mstari wa maombi unaopitia hapa, unatushikilia tukiwa salama kwenye ahadi. "Bila kuyumba-yumba, tukitupwa huku na huku, kwa kila upepo wa mafundisho. Bali tu salama, tusiotikisika, tukidumu siku zote katika neema ya Bwana, kadiri mjuavyo matendo yenu si bure katika Bwana." Ni tumaini lililoje!

122 Sasa, huyu Melkizedeki, tukinena tu juu Yake hapa, moja kwa moja. . .Paulo akizungumza na Waebrania, wa Agano la Kale, kwa mfano.

123 Hebu turudi kwenye Mwanzo, mlango wa 14, na kusoma kidogo tu kabla hatujaendelea, Melkizedeki huyu alikuwa Nani. Tunasoma katika mlango wa 14 wa Mwanzo, na kifungu cha 14, mwanzoni.

124 Ibrahimu, mnajua, alikuwa ameitwa kutoka Ukaldayo, nchi ya—ya Uru. . .mji wa Uru, hasa, nchi ya Ukaldayo. Naye Mungu akamwambia, "Jitenge na watu wako, na ujitenge." Hebu niweke mkazo juu ya hilo.

Loo, laiti tungelikuwa na wakati zaidi juu ya hili, leo! Ni mdogo sana.

125 "Jitenge na watu wako, na ujitenge, nami nitakubariki." Mnaona?

126 Na ili kupata ahadi iyo hiyo aliyo nayo Ibrahimu, huna budi kujitenga na mawasiliano yote ya kilimwengu, mambo yote ya ulimwengu. Shauku zako za dhambi, tamaa zako, hisia kali za

ulimwengu, na mambo haya yote, jitenge na kitu hicho. Jitenge, katika nchi ya kigeni, nchi ambayo hujawahi kufika hapo awali, ukatembee si kwa macho, bali kwa imani.

127 Kwa maana Ibrahimu hakuwa na kitu. Hakuna mtu aliyekuwa amevuka mto huu Frati na kukaa katika nchi hii. "Lakini Ibrahimu, kwa imani, aliwaacha walio wake, akaenda mbele, akijitenga."

128 Kama vile Damu ya Yesu Kristo, leo, kwa Roho Mtakatifu, inavyotutenganisha na mambo ya ulimwengu, kutembea katika maisha mapya; kukosolewa, kudhihakiwa, kuitwa "watakatifu wanaojifingirisha," kueleweka vibaya, lakini nanga yetu inashikilia.

129 Waebrania 11 ilisema, "Walizunguka-zunguka wakiwa wamevaa ngozi za kondoo na mbuzi, walikuwa wahitaji, na mahali pengi, kwa maana waliamini kwamba walikuwa wakiutazamia Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu." Kitu fulani ndani yao, kiliwaambia, "Kulikuwa na Nchi, Mji, Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Nao wakautafuta huo, wasijue waendako."

130 Ndivyo ilivyo kwa kila msafiri siku hizi. Anatafuta kitu ambacho hawezi kuweka mikono yake juu yake, lakini anaona ushahidi Wake umemzunguka pande zote. "Ni kitu gani kilichonifanya nifanye *hivi*? Ni kitu gani kilichomfanya mwanamke huyu kiwete kutembea? Ni kitu gani kilichomfanya mwanamke yule kiwete kutembea? Ni nini kinachoifanya hii henia kumwacha mwanaume huyu? Ni kitu gani kilichoifanya kansa hiyo kumwacha huyo mwanamke? Ni kitu gani kiliyafanya hayo masikio kiziwi kufunguka hivi majuzi usiku, hapa, umri wa miaka themanini na miwili? Nini kilichofanya hivyo?" Ni sifa za kimbinguni, kwamba ile nanga . . . Mji ule ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu, tunaoutazamia, hata hivyo hatuwezi kuona mahali ulipo, bali kuna kitu ambacho kinatia nanga huko ng'ambo. "Nanga ndani ya pazia. Matumaini yetu ni imara, yasiyotikisika."

131 Naye Ibrahimu akaiacha hiyo nchi, akakaa, akajiita mgeni na msafiri.

132 Na, tazameni, Ibrahimu, kama vile wanadamu wote; sio mwanadamu asiyepatikana na mauti, si mtu asiyeweza kufanya makosa, bali sikuzote alifanya makosa. Lakini haidhuru alifanya makosa mangapi, nanga yake ingali ilishikilia, kwa maana alikuwa na ahadi.

133 Kwa hiyo, alichukua pamoja naye, Sara. Akamchukua Lutu. Akamchukua baba yake. Na maadamu walikuwa pamoja naye, Mungu hangeweza kumbariki. Hatimaye huyo mzee akafa, wakamzika. Akaenda mbele kidogo, naye Lutu akarudi nyuma. Nanyi mnajua kilichotokea huko. Ndipo basi akajitenga naye. Ndipo Mungu akamtokea tena, akasema, "Sasa, Ibrahimu,

angalia kote nchini. Yote ni yako." Alipokuwa amefanya chaguo zuri. Ndivyo hivyo. Jitenge na kila kitu.

134 Itabidi niseme hivi. Tazameni. Natumaini litapata mahali pake pa kutulia, maana sikuwahi kuliwazia, kulitafakari awali.

135 Labda hiyo ndiyo sababu baadhi yetu hatuendani vizuri sana. Tunashikilia mambo ambayo tunapaswa kuyaachilia, katika utengano. Tashwishi kidogo, mshangao kidogo, shaka kidogo: "Sijui kama ni kweli. Hii inaweza kuwa? Je, Hiyo inaweza kuwa? Ingewezekanaje?" Jiweke huru, asubuhi ya leo!

136 Waebrania 12:1 inasema, "Na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi." Ile "dhambi," hiyo ni nini? Kule "kutokuamini" kunakotuzinga upesi. "Na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu, tukimtazama Kristo, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu."

137 Angalia Ibrahimu hapa. Ndipo, akapata shida, Lutu akashuka Sodoma na Gomora. Mnaijua hiyo hadithi.

138 Itatubidi kuharakisha, tumebanwa. Hatuwezi kukifikia. Kifungu cha 14.

139 Basi muda si muda mwajua, wafalme wote wa Mataifa wakashuka kule, wakaja Sodoma na kutangaza vita, wakamtwaa Lutu, na mpwawe Ibrahimu, wakamchukua, Mke wa Lutu, na watoto, na hao wengine wote, na kuondoka nchini.

140 Basi mmoja wa wafalme wa Sodoma, alipoanza kukimbia, aliingia kwenye mashimo ya lami huko nje, naye akatumbukia akafa. Lami ndiyo walitengenezea matofali yao na chokaa, ndipo wakajenga miji yao kwayo.

141 Kwa ajili ya utangulizi mdogo wa kusoma hili. Unaweza kulisoma ukifika nyumbani. Lakini kwa sababu ya upungufu wa wakati, itabidi tuharakishe. Na kifungu cha 14:

> *Abramu aliposikia ya kwamba ndugu yake amechukuliwa mateka,*. . .

142 Ndugu, napenda hilo, "ndugu yake," halafu angalia yale Lutu aliyokuwa amemfanyia! Lakini, hata hivyo, kulikuwa na namna fulani ya kifungo kifungacho, kama huyo ndugu amerudi nyuma. Kama vile huyu kijana alivyosema muda mfupi uliopita, huyu mhudumu kijana hapa, ya kwamba alikuwa amerudi nyuma na kwenda zake. Hata hivyo, kwa namna fulani, Roho Mtakatifu bado anamwita mtu huyo. Anapokuwa katika shida, Yeye yuko papo hapo pamoja naye.

> . . .*Nduguye* Ibrahimu *ametekwa mateka, akawapa silaha watumishi wake waliofunzwa,* naye akawachukua juu ya ninii yake. . .*waliozaliwa katika nyumba yake, mia tatu na kumi na wanane, akawafuatia mpaka Dani.*

*Naye akajipanga apigane nao, usiku yeye na watumishi wake,. . . akawapiga, na kuwafukuza mpaka Hoba,* ulioko *upande wa kushoto . . . kwenda Dameski.*

143 Ibrahimu akawachukua watumishi wake wote na watu wenye silaha. Hebu fikiria tu mtu aliyekuwa maskini hohehahe alipoiacha ile nchi kule Ukaldayo, wa Uru, alikuwa na watu mia tatu na kumi na wanane wenye silaha kama watumishi. Ati wasema Mungu hakubariki? "Mia tatu na kumi na wanane."

Unasema, "Vema, hiyo ni kweli?"

144 Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. Alikuwa na watumishi wa kutosha kupigana na jeshi. Naye akapata ushindi! Angalieni, "Naye akarudisha . . . " Akawafukuza; akachukua kila kitu walichokuwa nacho.

*Na . . . alirudisha mali zote, na pia akamrudisha Lutu nduguye, na mali zake, na wanawake pia, na watu.*

*Na mfalme wa Sodoma akatoka amlaki baada ya* kurudi *kutoka katika kuwapiga* . . . na wafalme . . . wa— wa lile *bonde* . . . na *bonde la mfalme.*

*Naye Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai,* akampa: *naye alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu.*

145 Baada ya wafalme hawa wote wa Mataifa kuingia na kumchukua ndugu yake, Ibrahimu aliwachukua watumishi wake, akawafuatilia, akashuka, akawachukua; kisha akarudi pamoja nao (na wafalme aliowapiga), na kuwarudisha.

146 Basi, angalieni, mfalme wa Sodoma akatoka. Mfalme wa Gomora aliuawa. Lakini mfalme wa Sodoma akatoka, akamleta huko, na kusema hapa, "Mali zote u—ulizotwaa, ambazo watu hawa walichukua, nitakupa wewe."

147 Baadaye, katika mlango huu, tunaona Ibrahimu alisema, "Sitatwaa uzi, wala gidamu ya kiatu; usije ukasema ulimtajirisha Ibrahimu."

148 Lakini wazo tunalotaka kufikia, liko papa hapa.

*Naye Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu.*

*Akambariki, akasema,* Ibrahimu *na abarikiwe na Mungu aliye juu sana, Muumba* mbingu *na nchi:*

*Naye akambariki, na yeye . . .*

*Na ahimidiwe Mungu aliye juu, aliyewatia adui zako mkononi mwako. Naye akampa* fungu la kumi *la vitu vyote.*

149 Naipenda. Angalieni sasa, baada ya Ibrahimu, ile picha ya kiroho hapa, Ibrahimu; "ndugu yake" ambaye alikuwa amepotea. Picha ya Kanisa la kweli, ama mwaminio wa kweli wa

Mungu, aliyebarikiwa na Mungu, na aliye na ahadi ya Mungu, aliye na agano la Mungu, na ana imani katika agano.

150 Sasa wazia. Kama utahesabu hapa, kulikuwa na yapata wafalme kumi au kumi na watano walikwenda kule, na, pengine, walikuwa na watumishi wangapi?

151 Lakini Ibrahimu alihesabu wale aliokuwa nao ambao walikuwa waaminifu, "waliozaliwa katika nyumba yake mwenyewe." Loo, jamani! Waaminifu, "waliozaliwa katika nyumba yake mwenyewe." Walikuwa watumishi wake ambao alikuwa amewatahiri, ambao walijumuishwa katika ahadi ile ile aliyokuwa nayo. Naye akamfuatilia nduguye aliyerudi nyuma, akamfuatilia kwa kundi dogo la watu, watu mia tatu na kumi na wanane; akawafukuza wale wafalme, akawashinda, akawashika na kuwaua. Na kurudisha yote yaliyokuwa yamepotea.

152 Picha kamili ya Kristo! Na Kanisa, Roho Mtakatifu akiwaongoza waaminifu waliozaliwa katika nyumba ile ile ya Roho Mtakatifu ambamo Kristo alizaliwa, akiwafuatilia waasi na waliorudi nyuma. Na kuua kila uovu uliowashinda. Amina! Kushinda dhambi, kuweka kando mizigo yote. Kuzungumza na watu juu ya tamaa zao mbaya na mambo wanayofanya; kuyakatilia mbali! Magonjwa yao na yote; kuwahubiria Injili, na kuwarudisha katika ushirika mkamilifu pamoja na Mungu.

153 Angalieni. Basi aliporudi, Melkizedeki akakutana naye. Huyu Melkizedeki alikuwa ni nani? Pia angalieni, jambo la kwanza, sasa. Melkizedeki hakumpa pesa yoyote. Melkizedeki alimtolea tu "mkate na divai." Melkizedeki alikuwa Kuhani wa Aliye Juu Sana; mfalme wa Yerusalemu.

154 Wakati huo uliitwa Salemu. Hii hapa Cruden. Niliwazia, kama lingeuliziwa baadaye, ninaweza kulithibitisha, ya kwamba Yerusalemu ulikuwa kwanza Salemu. J-e-r-u-s- -l-e-m, mnaona, Salem, Jeru-salem. Mnaona? Kwanza uIiitwa H-i- -r-u- -a- -m, Hieru-salem, hiyo ni kweli, ambao, wakati ulipokuwa katika milki ya Mataifa. Loo, natumaini mnalipata hili sasa. Yerusalemu kwanza ilikuwa mikononi mwa Mataifa.

155 "Naye Mfalme wa Yerusalemu, au Salemu, ambalo lilimaanisha Mfalme wa amani, Mfalme wa haki, alikutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi. Na kumpa," ushirika, "mkate na divai," maelfu ya miaka, au mamia ya miaka, kabla ya mkate na divai kupata kuwa maagizo Kanisani. Naye alikuwa ni Mfalme wa Yerusalemu. Amina.

156 Mtu huyu mkuu alikuwa nani? Turudi kwenye somo letu sasa, kifungu cha 7 . . . au, mlango wa 7.

> *Kwa maana Melkizedeki huyu, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, . . .*

157 Hakuwa tu Mfalme, bali alikuwa Kuhani.

*. . . aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;*

158 Baraka hutoka tu kwa mtu aliye mkuu zaidi. Tazama. "Ambaye ni-. . ."

*Ambaye Ibrahimu alimpa sehemu ya kumi ya vitu vyote;* kwanza *tafsiri yake ni Mfalme wa haki, . . . baada ya hapo . . . Mfalme wa Salemu, yaani, Mfalme wa amani;*

159 Mtu huyu mashuhuri alikuwa ni nani miaka mingi, mingi iliyopita? Alikuwa Nani? Sikilizeni. Hebu tusome zaidi kidogo juu Yake.

*Bila baba, bila mama, . . .* bila *mwanzo wa siku,* au bila mwisho *wa maisha; . . .*

160 Kama hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku wala mwisho wa maisha, Melkizedeki angali yupo. Hiyo ni kweli? "Alifanywa kwa mfano . . . Akiwa hana baba, hana mama."

*. . . bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; huyo adumu kuhani milele.*

161 Hawezi . . . Hakuwa na mwanzo. Hana mwisho. Hakuwa na baba. Hakuwa na mama. Hata hivyo, Yeye alikuwa Mwanadamu, Naye alitoka Salemu. Amani, alikuwa Mfalme wa amani. Alikuwa Mfalme wa haki.

162 Yeye hakuwa Mfalme tu, bali alikuwa Mtawala. Naye ni Mfalme wa Amani. Yeye ni Ua la Uwandani. Yeye ni Yungiyungi la Bondeni; Nyota ya Asubuhi; Alfa, Omega; Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi pia. Alikuwa kabla ya Daudi, ndani ya Daudi, na baada ya Daudi.

163 Kuhani huyu alikuwa nani? Si mwingine ila Bwana Yesu Kristo aliyefanyika mwili, katika uweza Wake mkuu sana. Alikuwa ni Yeye yule, baadaye kidogo, baada ya kukutana na Ibrahimu. Naye akampa, kwa kuwa ni watu wa agano, ushirika. Ndipo, sasa, kupitia agano lilo hilo, tunachukua . . . Naye alikuwa katika kivuli. Melkizedeki huyo, alipofanyika Mtu wa mwili, angekatwa vipande. Ndipo ushirika utatolewa, manukato ya mwili Wake uliovunjwa, kama tunavyoula siku hizi.

164 Hapo Melkizedeki huyo alikutana na Ibrahimu, naye Ibrahimu akampa fungu la kumi. Amina. Ibrahimu, mtu mkuu zaidi juu ya uso wa dunia, alimpa Melkizedeki fungu la kumi: Mfalme wa amani, Mfalme wa Salemu, Mfalme wa haki.

165 Naye alikuwa Mtawala. Na Yeye alikuwa—Yeye alikuwa Mtawala. Alikuwa Mfalme. Naye alikuwa Mtumishi wa Aliye Juu Sana, ambaye alikuwa ni Yesu.

166 Basi wakati Ibrahimu, miaka michache baadaye, ama si muda mrefu baada ya hayo, wakati Lutu alipokuwa amerudi nyuma, nayo Sodoma imeteketezwa. Naye Ibrahimu akaachwa peke yake, pamoja na Sara, huko nje kwenye nchi kame. Wakati kulikuwa. . .Ng'ombe wao wote walikuwa wakifa, kutokana na njaa. Na ilionekana kana kwamba Mungu alikuwa amempungukia. Lakini alikuwa na imani thabiti, kuamini.

167 Basi siku moja alikuwa ameketi katika mlango wa hema yake, chini ya mwaloni mkubwa. Bado ungali umesimama kama kumbukumbu leo hii, kwa kuwa umeunguzwa na kushikiliwa. Na hapo, Ibrahimu, huku ameketi mlangoni pa hema yake, alimwona Melkizedeki akimjia; Wanaume watatu wakitembea.

168 Nami ninamwazia tu Ibrahimu akisema, "Nimemwona hapo awali." Naye anakaribia. Ndipo akasema, "Naomba nininii tu. . .Njoni, Bwana wangu, na uniruhusu nilete maji kidogo kwa ajili ya miguu Yenu." Kwa namna fulani, huko chini kabisa, mtu huyo wa agano, chini moyoni mwake, alijua ya kwamba Huyo alikuwa ni Mtu fulani zaidi ya mwanadamu.

169 Akasema, "Sisi ni wageni." Kasema, "Tumetoka nchi ya kigeni." Nguo zao zilijaa mavumbi. Naam, walitoka, kote kutoka Utukufuni. Na kwa hiyo walienda kule, na kumwambia Ibrahimu. . .Wakawaletea kitu kidogo, nao wakanawa. Ndipo Ibrahimu akaanza kuwaangalia.

170 Akarudi upesi ndani ya hema, na kusema, "Sara, simama hapa kwa dakika moja." Akatoka kupitia kwenye kundi, akachukua ndama aliyenona zaidi ambaye angeweza kumpata. Naye akamchinja, na kumleta.

171 Ndipo akampa Mtu huyu nyama, na mkate, na maziwa, na siagi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .kula.

172 Sasa, wakati Melkizedeki, mfalme wa Salemu, kuhani wa aliye Juu Sana, Mfalme wa amani, ambaye hakuwa mwingine ila kuonekana kimbele kwa Bwana Yesu Kristo. Naye alipokutana na Ibrahimu, alimlisha Ibrahimu ushirika, kisha akambariki. Na hapa yeye, Ibrahimu, anakutana Naye akienda zake Sodoma, na kumlisha nyama na mkate.

173 Loo, hivi hamwoni uhusiano kati ya hao wanaume? Yeye aliahidi. Mkate wetu na maji ni hakika. Naye Mungu atafanya jambo hilo, hakika tu kama tunavyoketi hapa. Na kila ahadi ya Kiungu aliyoitoa, Yeye anawajibika kuitimiza.

174 Basi wale Malaika wawili walipoelekea Sodoma, Ibrahimu alisimama pale. Naye akatazama huku na huku, pamoja na huyo Mtu. Akasema, "Endapo nitapata *kadhaa* na *kadhaa*," kama alivyoendelea kusema, kufikia kumi. Ndipo alipoondoka; basi Malaika, au Mtu aliyekuwa amesimama karibu naye, akatoweka na kutokomea, karibu na ile dhabihu. Ndipo Ibrahimu akasema, "Nimezungumza uso kwa uso na Mwenyezi Mungu." Melkizedeki, na, Kristo katika utangulizi.

175 Jinsi ambavyo, enyi marafiki, asubuhi ya leo, kama tungeweza kuchukua pazia hili hapa, lililo mbele ya macho yetu, kwa kuwa mwili umetupofusha, na kupasua pazia hilo namna *hii* na kuangalia tu ng'ambo ya pazia la wakati, kustaajabu ingekuwaje. Nilizoea kuimba wimbo mdogo:

> Nimevunjika moyo na kuhuzunika, nami ninataka kumwona Yesu.
> Ninataka kusikia zile kengele tamu za bandarini zikilia.

Naam, laiti ningaliweza kumwona Yeye, na kutazama tu ng'ambo ya pazia la wakati.

> Ingenipa . . . imani zaidi, na ningefanya yote, na kufanya nguvu zangu zote,
> Iwapo tu ningeweza kutazama ng'ambo ya pazia la wakati.

176 Huyo alikuwa ni nani pale, katika Yerusalemu hii duniani papo hapo basi, "Ambaye hakuwa na mwanzo wa siku, wala mwisho wa miaka," na akaja na kumpa ushirika Ibrahimu ambaye alikuwa na ahadi? Nayo ahadi imeletwa kwetu, asubuhi ya leo. Ni kwa kila mmoja wenu.

177 Tungeweza kuwa na muda zaidi, laiti tungelikuwa nao, juu ya somo hili kuu; labda siku moja, baada ya safari hii kuisha.

178 Ninapozunguka mataifa sasa, katika nchi za kigeni na kandokando, nikihubiri Injili, hebu niwaachie wazo hili, watoto wangu wapendwa, ndugu zangu na watenda kazi wenzangu katika Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Msichoke. Pateni ujasiri mpya asubuhi ya leo. Inueni vichwa vyenu. Inueni magoti dhaifu na mikono ambayo wakati mmoja ilining'inia chini. Mwangalieni Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, Bwana Yesu Kristo, Yeye aliyetupa ahadi hizi. Jambo hili ambalo nimejaribu kuwahubiri ninyi kwa ufunuo niliopewa na Bwana Yesu Kristo, wakati ningali sina elimu wala sijasoma, sina kisomo, hata hivyo Mwenyezi Mungu ameliweka mbele ya ulimwengu, kwa kuwa haliwezi kukosea.

179 Huku wameketi hapa, asubuhi ya leo, ni wale ambao walikuwa vilema na wanaoteseka, juma lililopita, na juma hili ni wazima na wenye afya. Kuna wale waliokuwa viziwi, wamesimama hapa siku chache zilizopita usiku; wamesimama hapa sasa, wakisikia vizuri tu kama hao wengine. Ni nini? Ni agano la Mungu lisilo na masharti alilofanya na Ibrahimu na Uzao wake. Aliahidi angefanya hivyo, kwa hiyo basi na tuamini asubuhi ya leo kwa moyo wetu wote.

180 Kama watu, wengine wetu wanaoketi hapa, wazee, wengine wetu wakiingia mvi. Baadhi yetu, kabla hatujakutana tena, kunaweza kuwa na baadhi yetu watakaopita ng'ambo ya pazia. Lakini lolote mfanyalo, lolote maisha yaletalo, kama yakileta maradhi, kama yakileta lolote duniani, dumisha nanga

yako ndani ya pazia. Endelea kumwangalia Mwandishi na Mkamilishaji huko ng'ambo, Bwana Yesu Kristo. Viite vitu hivyo, vinavyoonekana kuwa, kana kwamba vilikuwepo.

181 Kuna mambo matatu ambayo mtu hufuata. Kwanza, ni ya kibinadamu; pili, ni ufunuo wa Kiungu; tatu, ni ono, ni BWANA ASEMA HIVI. Mara nyingi, tuko chini *hapa* ndani, wala kamwe hatupandi kuingia katika *hili*. Kama huko kule chini, tupa matumaini yako kupitia hilo pazia, hapa juu kwenye BWANA ASEMA HIVI. Ingawa huoni ono; ingawa ufunuo hauji; ingawa, unapoombewa, unasema, "Laiti tu ningeweza kuamini." Hilo halileti tofauti yoyote. Itie nanga yako kule chini, na uiite hivyo, kwa vyovyote vile.

Ibrahimu hangeweza kuona. Alisema, "Inawezekanaje?"

182 Mariamu asingeweza kuelewa. Angewezaje kupata mtoto, "bila kumjua mwanamume"?

183 Alisema, "Lakini Roho Mtakatifu atakujilia juu yako. Atalitimiza."

184 Alisema, "Tazama mjakazi wa Bwana. Iwe kwangu." Je, ingefanywaje? Yeye hakujua. Lakini alitupa nanga yake ng'ambo ya pazia, kisha akatoka akishuhudia kwamba alikuwa anaenda kupata mtoto, kabla hajahisi uhai ama chochote kile. Aliviita vile vitu ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwepo.

185 Ibrahimu, alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, Mungu alimpa ahadi. Naye Sara, mwenye umri wa miaka sitini na mitano, alitoa ahadi. Ndipo miaka ishirini na mitano ikapita kabla haijatimia. "Lakini Ibrahamu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa hodari katika imani, akimtukuza Mungu. Na kuziita hizo dalili, na vitu vilivyokuwako, kana kwamba havikuwepo." Na kushuhudia tu yale Mungu aliyosema ni kweli, kwa sababu alikuwa na ahadi.

186 Mungu aturehemu. Loo, jamani! Je, imani yako imetulia kimya asubuhi ya leo? Wakati pepo za shida zinapovuma, usiku una giza, na pepo na radi zinamulika, je, nanga yako inashikilia? Jenga matumaini yako asubuhi ya leo si juu ya kitu kingine chochote ila Damu ya Yesu pamoja na haki. Najua ni ngumu. Inaonekana ngumu. Lakini lichukue wakati mmoja, na umwamini Mungu kwa Neno Lake, ndipo uone ni tumaini la baraka jinsi gani kusonga mbele tu kwa imani.

187 Katika vita hivi vikuu vya imani, kama vile nimejaribu kuvipiga, nimekutana na pingamizi kali, nimepitia barabara mbovu. Nina dalili zake. Ninazo. Lakini limekuwa jambo la baraka sana. Nisingelibadilisha kwa chochote kile ulimwenguni.

188 Basi huu hapa ushindi wangu mkuu, raha kuu sana nilizo nazo, ni wakati ninapokabiliana na jambo fulani. Siwezi kuona juu yake, kando yake, au chini yake. Ninaendelea tu kuliendea, nikiamini jambo hili, ya kwamba Mungu atafanya

njia nitakapofika pale. Sijawahi kuja mwaka huu, umbali huu, ninii. . .Na umbali huu wote nimefikia, nimemwamini Yeye. Hajawahi kunipungukia.

> Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
> Neema ndiyo iliyoondoa hofu yangu;
> Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
> Ile saa niliyoamini kwanza!
>
> Na kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,
> Nimekuja tayari;
> Ni neema ambayo imenileta salama umbali huu,
> Neema ndiyo itakayonipeleka.
>
> Na wakati tumekuwa huko miaka elfu kumi,
> Tuking'aa sana kama jua;
> Hatutakuwa na siku pungufu kuimba sifa Zake
> Kuliko tulipoanza kwanza.

189 Tunapokusanyika Huko, pamoja na Ibrahimu, Isaka na Yakobo, wale waliokuwa warithi wa ile ahadi, wakitazamia tusishindwe, "kwani bila sisi hawawezi kukamilishwa." Na jinsi wanavyotutegemea sisi, asubuhi ya leo! Hebu tusishindwe. Dumisha nanga yako katika Kristo.

190 Ikiwa wewe ni mwenye dhambi, si lazima uje madhabahuni. Ni desturi kufanya hivyo. Lakini ikiwa hutaki kuja, na hakuna nafasi kwako kuja, sema, "Bwana, ninatupa mambo yote ya ulimwengu kando, sasa hivi. Ninajilaza mbele Zako, wazi na tupu jinsi nilivyo, nami ninaona aibu na fedheha. Lakini ninatupa nanga yangu Kwako. Nami nakuamini Wewe. Hakuna ninachoweza kufanya ila kile ambacho umenifanyia Wewe."

191 Ikiwa wewe ni mgonjwa, daktari anasema hakuna njia hata kidogo kwako kuwa mzima, hakuna kinachoweza kufanywa. Angalia tu kwenye hii maska-. . .kundi hili dogo la watu asubuhi ya leo, wakati, hili ni ku—kundi dogo, hata si nukta moja ya maelfu ambao wameponywa katika majuma haya machache yaliyopita, kote ulimwenguni.

192 Miamsho mikubwa! Ulimwengu uko katika kishindo, pamoja na miamsho ya uponyaji wa Kiungu; watu wa imani wakitoka nje, wakithubutu kuliamini Neno la Mungu. Siku za Mataifa zinaisha. Hii ni ishara. Iangalie. Usingojee muda mrefu sana.

193 Walingoja muda mrefu kupita kiasi, kumtambua Eliya. Nao wanafunzi hata wakasema, "Kwa nini waandishi wanasema, 'Eliya hana budi kuja kwanza'?"

Akasema, "Amekuja tayari, wala hamkumtambua."

Kasema, "Alikuwa ni nani?"

Kasema, “Yohana Mbatizaji.”

“Vema,” wakasema, “hakika, huyo alikuwa ndiye.”

194 Yesu alikuja, nao hawakujua. Baada ya Mrumi kumsulubisha, wakati ilipokuwa imechelewa sana kufanya lolote, yeye alisema, “Kweli huyo alikuwa Mwana wa Mungu.” Ingawa alikuwa mhalifu, ingawa ali—alitemewa mate, ingawa alidhihakiwa na kuteswa, hata hivyo Mungu alimthibitisha kwa ishara na maajabu.

195 Leo, tusisubiri sana. Huu ndio mwisho wa kipindi cha Mataifa. Tunamalizia.

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
> Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
> “Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”
>
> Siku ya ukombozi imekaribia,
> Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
> Mjazwe na Roho, taa zenu zikiwa zimesafishwa na kuwa safi,
> Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

196 Baba yetu, tunakushukuru Wewe asubuhi ya leo kwa ajili ya tumaini hili lenye baraka. Loo, siku fulani tukufu, utakaposimama juu ya nchi tena, itasemwa, “Je, haikuandikwa katika nyimbo, ‘Ukombozi wenu unakaribia’?” Ulipokuwa hapa mara ya kwanza, ulisema, “Je, haikuandikwa na Daudi, katika nyimbo, mambo fulani haya?”

197 Na tunapoukumbuka wimbo huo, “Kutakuwa na mkutano hewani,” kwa maana manabii wote, na waliokombolewa, na maskini Daudi, na Musa, na wazee wetu wote, watakuwepo Huko. Ndipo tutasema, “Je, haikuandikwa kwenye ule wimbo, kwamba tungeona hili?” Nao waliokombolewa wa nyakati watashangilia pamoja.

198 Baba, msamehe mwanamume au mwanamke mpotovu, mvulana au msichana asubuhi ya leo. Jalia hii iwe siku mpya maishani mwao, wakati ambao, kwa imani, wanamkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wao binafsi na kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, na Roho Mtakatifu.

199 Yachukue maneno haya machache, yaliyoharakishwa, Baba, na uyazamishe ndani ya mioyo ya watu, kulingana na mahitaji yao.

200 Katika muda mfupi tu sasa, watu watapitia hapa, wapate kuponywa. Kutakuwa na hao hapa, Bwana, ambao ni vipofu, wanaoteseka, na viwete, na wagonjwa, na magonjwa ya kila namna juu yao. Shetani amefanya jambo hili ovu, Baba. Maskini watu hao, Bwana, hawangekuja hapa kama hawakuamini wangeweza kuponywa.

201 Wewe ulisema, "Tunashinda kwa Damu ya Mwana-kondoo pamoja na ushuhuda wetu." Na hapa kuna nyuzi zimewekwa hapa jukwaani. Magongo na kadhalika yamelundikwa, na kukokotwa kutoka hapa; na viti vya magurudumu, na, loo, machela yamebebwa yakaondolewa, na vitanda. Na wanaume na wanawake wametembea kutoka hapa, Bwana, kutokana na kila namna ya magonjwa na mateso ambayo Shetani alikuwa ameweka juu yao. Si kwa sababu ni mahali hapo, bali ni kwa sababu imani yao ilikidhi mahitaji Yako papa hapa.

202 Ninaomba, Mungu, ya kwamba kila mgonjwa humu ndani, kwamba imani yao itatosha, asubuhi ya leo, sasa, kumkumbuka yule Melkizedeki mkuu kule nyuma, Ambaye hakuwa na mwanzo wa siku. Kamwe hakuwa na baba, wala mama. Hakuwa na mwisho wa uhai; ambaye bado yu hai leo. Kisha, akafanyika mwili, ulioitwa Yesu Kristo, akawa mwili; akafa na kuurudia tena. Yeye angali ni Mfalme wa amani, Mfalme wa haki, akituahidi mambo haya makuu ya Milele. Ambaye Yeye... Imeapiwa na Mungu, kwa Ibrahimu, ya kwamba atalitimiza lile agano, ahadi, kupitia Yeye na Uzao Wake, milele. Tusaidie, leo, kusonga mbele kwenye jukwaa hili sasa, pamoja na imani isiyo na kikomo.

203 Baadhi yao hapa, Bwana, wamefungwa na tabia chafu, maskini tabia chafu za mwili. Mungu, kama Biblia ilivyosema, "Na tuweke kando kila mzigo, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi." Mungu, na waitupe kando, asubuhi ya leo, na kumtazama Yesu anayetusafisha na udhalimu wote. Tujalie, Baba.

204 Na tukiondoka leo, jalia twende kwa moyo uliojaa upendo, na kushangilia. Libariki kanisa hili dogo. Mbariki Ndugu yetu mpendwa Neville, Bwana, anapofanya uchungaji, na kushughulika mchana na usiku hapa, akijaribu kuandaa ma—mahali kwa ajili ya watu kuja kuabudia, kumwona Bwana Yesu katika udhihirisho Wake wa upendo na nguvu.

205 Ibariki ibada ya usiku wa leo, Bwana. Lete baraka kubwa kwetu. Pia, Baba, tunaomba sasa ya kwamba utapata utukufu kwa mambo yote.

206 Na siku moja, wakati maisha yote yamekwisha, mahubiri ya mwisho yamehubiriwa, Biblia imefungwa; ishara za kuzima taa jeshini zimetolewa, silaha zimelundikwa, moshi wa vita unafifia, jua linatua; basi, Baba, utupokee katika Ufalme Wako. Jalia tuje kama askari wastaafu wenye makovu ya vita. Tujalie, Bwana, ili tuweze kupokea mwili mpya, ambapo hatutakuwa wagonjwa tena, wala kuwa na sikitiko au huzuni.

207 Lakini jalia tuwe waaminifu katika mambo haya yote, wakati tukiwa hapa duniani sasa, kuamini, na kuviita vitu hivyo visivyokuwako, ambavyo ni kinyume na Neno la Mungu, kana kwamba viko. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

208 Mtu yeyote hapa angejisikia, kusema, “Ningependa tu kumkubali Bwana Yesu Kristo. Sijawahi kufanya hivyo hapo awali. Nataka tu kuinua mkono wangu.” Niseme, “Mimi, kwa kuinua mkono wangu, ninamkubali.” Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni. . . Mungu akubariki, ndugu. “Ninataka kumkubali Bwana Yesu Kristo.” Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Na Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni sawa.

209 Mnafikiri Yeye hasikii hilo? Anaujua moyo wako. Yeye ndiye aliyekwambia ulifanye. Mtu mwingine aseme, “Sa—sasa nataka kuamini. Sa—sasa nasema, ‘Bwana, nataka kukukubali sasa hivi. Nataka nanga yangu ikazwe, kule kwenye pazia, isije ikasogea kamwe. Ninakukubali Wewe kama Mwokozi wangu.’” Je, unaweza kuinua mkono wako, mtu mwingine? Mungu akubariki.

> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Vipi basi?
> Wakati kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, vipi basi?
> Wakati wale wanaoukataa Ujumbe huu leo,
> Wataulizwa kutoa sababu-Vipi Basi?

210 Bwana na awabariki sasa. Wakati ninyi. . . tutakuwa na. . . Ni wangapi hapa watakaoombewa, walio wagonjwa? Hebu tuone mikono yenu, mahali popote kwenye jengo, walio wagonjwa.

55-0109M Melkizedeki, Yule Mtawala Mkuu na Mfalme
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org